JINA LA MTAHINIWA ……………………………………………………. ………………………… JINA LA SHULE……………………………

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA KILIMANJARO

MTIHANI WA MHULA WA II – DARASA LA III

05

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Muda: Saa 1:30 **November 2024**

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **matano(5)**
2. Jibu maswali **yote**.
3. Onesha wazi njia zilizotumika kujibu maswali yote katika nafasi iliyotolewa kwenye karatasi ya maswali.

SEHEMU A

1. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi hiyo katika kisanduku ulichopewa.

i. __________ ni mfano wa kiumbe ambacho mwili wake umesawazishwa na kufunikwa na manyoya.
   A. Mbu
   B. Tai
   C. Mbuzi
   D. kipepeo.

ii. Kuna aina ___________ za maada.
   A. Tatu (3)
   B. Nne (4)
   C. Mbili(2)
   D. Tano (5)

iii. Hatua ya kwanza katika kufanya uchunguzi wa kisayansi ni __________
   A. Kubuni dhanio
   B. Hitimisho
   C. Kubaini tatizo
   D. Kuandika taarifa

iv. Sauti inayojirudia huitwa ______________________________
   A. Kuakisiwa
   B. Wimbi
   C. Mwangwi
   D. Mwanga

v. Mtu anayeshughulika na utafiti wa kisayansi wa mimea anaitwa_______________
   A. Daktari wa wanyama
   B. B.Mtaalamu wa mimea
   C. C.Mkemia
   D. D.Mfamasia

SEHEMU B

JINA LA MTAHINIWA ……………………………………………………. ………………………… JINA LA SHULE……………………………

2. Mwanasayansi mchanga aliliunganisha vitu vifuatavyo kwa usahihi, majibu yake yalikuwa nini?

ORODHA A	**MAJIBU**	**ORODHA B**
i. Wanavuta gesi ya oksijeni		A. Samaki
ii. Ni mfano wa mamalia anayeruka		B. Ukuaji
iii. Hali ya viumbe hai kuongezeka kimo na uzito		C. Wanyama
iv. Utumia matamvua kupumua		D. Ndege
v. Ni mnyama mwenye damu joto		E. Kujongea
		F. Popo

SEHEMU C

3. Chagua neno sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha ujaze nafasi zilizoachwa wazi.

Kuzaliana , kipima joto, mionzi , kujongea , mnururisho , hewa , Ngozi , pua

i. Joto kutoka kwenye jua hufika kwenye uso wa dunia kwa njia ya ______________.
ii. Mchanganyiko wa gesi mbalimbali huitwa _________________.
iii. Viumbe hai huongezeka kwa njia ya ______________.
iv. Kifaa kinachotumika kupima halijoto _________________________.
v. Ogani inayotumika kuhisi _________________.

SEHEMU D

4. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

Sikio ni ogani inayotuwezesha kusikia. Sikio lina sehemu kuu tatu. Sehemu ya nje,sehemu ya kati na sehemu ya ndani. Sehemu ya nje hukusanya mawimbi ya sauti na kuyaelekeza kwenye sehemu ya kati ya sikio.Sehemu ya kati ya sikio hupokea mawimbi ya sauti kutoka kwenye ngoma ya sikio na kuyapitisha sehemu ya ndani ya sikio. Sehemu ya ndani ya sikio husafirisha mawimbi ya sauti mpaka kwenye ubongo ili yatafsiriwe kama sauti.

MASWALI

i. Sikio ni ogani inayotuwezesha _____________________________

ii. Sehemu ya nje ya sikio hukusanya mawimbi ya sauti na kuyaelekeza kwenye __________________ kwa kupitia ngoma ya sikio.

iii. Ni sehemu gani ya sikio hupokea mawimbi ya sauti kutoka kwa ngoma ya sikio_____________

iv. Ni sehemu gani ya sikio inayoruhusu kupitisha mawimbi ya sauti kwenda kwa ubongo

v. Pendekeza kichwa kinachofaa kwa kifungu ____________________________

SEHEMU E

5. Tazama picha hapo chini kisha ujibu maswali yanayofuata.



MASWALI

i. Taja vifaa vyovyote viwili vya TEHAMA vilivyoonyeshwa kwenye mchoro hapo juu
(A)_______________________________

ii. (B)_______________________________

iii. Vifaa hivi huweza kupatikana maeneo kama _______________________________

iv. Taja kifaa cha TEHAMA kilichotumika kwenye picha iliyoandikwa herufi D ______________

v. Simu janja imeandikwa kwa herufi ipi? _______________________________

vi. Andika faida moja ya kucheza michezo ya TEHAMA _______________________________